HOTUBA YA MHE. DKT. DOTO MASHAKA BITEKO (MB.) WAZIRI WA MADINI KATIKA UFUNGUZI WA MKUTANO MKUU WA MWAKA WA JUMUIYA YA WAJIOLOJIA TANZANIA (TANZANIA GEOLOGICAL SOCIETY (TGS)), OKTOBA 04, 2022.

Mhe. John Vianney Mongela – Mkuu wa Mkoa wa Arusha,

Waheshimiwa Manaibu Waziri mliopo,

Makatibu Wakuu Mliopo,

Bw. Msafiri Lameck Mbibo – Naibu Katibu Mkuu Madini,

Manaibu Katibu Mkuu Mliopo,

Prof. Abdulkarim Mruma – rais wa Jumuiya ya Wajiolojia Tanzania,

Dkt. Joas Kabete – Makamu rais wa Jumuiya ya Wajiolojia Tanzania,

Dkt. Elisante Mshiu – Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Wajiolojia Tanzania,

Ndugu wanajumuiya ya Wajiolojia Tanzania,

Ndugu waheshimiwa wote mliofika hapa leo,

Ndugu wageni waalikwa,

Waandishi wa habari, Mabibi na mabwana……………….!

Walsaam aleykum, Bwana Yesu asifiwe ……………………..!

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania……..!



Edit with WPS Office

Awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kumshukuru mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa afya aliyotujalia hata tukaweza kukusanyika mahali hapa siku ya leo. Aidha, namshukuru Mhe Dkt. Philip Mpango, kwa kunituma kumuwakilisha katika tukio hili muhimu la uzinduzi wa Mkutano Mkuu wa Mwaka 2022 wa Jumuiya ambayo hufanyika kila mwaka. Niwashukuru pia Jumuiya ya Wajiolojia kwa kuandaa mkutano huu muhimu.

**Ndugu Wajiolojia**,
Jiolojia ni sayansi ya dunia ambayo inagusa kila nyanja za maisha ya mwanadamu. Natambua mnajifunza kuhusu miamba, ambayo elimu hiyo inatoa fursa mbalimbali. Mfano, tunaendesha kilimo kutokana na uwepo wa udongo ambao asili yake ni miamba, tunakunywa maji yatokayo ardhini kwenye mifumo ya miamba, tunatumia metali mbalimbali katika viwanda vyetu vya uzalishaji, metali hizi zinazotokana na madini yaliyomo kwenye miamba.
Pamoja na hayo yote, baadhi ya vyanzo vya nishati tunavyotumia vinahusiana moja kwa moja na Jiolojia. Mfano, joto ardhi, mafuta na gesi asilia, makaa ya mawe na madini ya Urani (Uranium). Hivyo, jiolojia ni sayansi muhimu kwetu kama wanadamu na kama nchi, watu wetu wanapaswa kuendelea kuutafuta utaalamu huu ili uchangie maendeleo ya nchi yetu.

**Ndugu Wajiolojia,**
Ukiacha kilimo, rasilimali zilizopo kwenye miamba ikiwemo madini, vito, mafuta na gesi asilia ndizo zenye mchango mkubwa katika malighafi za viwanda kote duniani na kama nilivyosema hapa kwetu tumebarikiwa sana kwa rasilimali hizi. Miamba na madini mbalimbali ina matumizi mengi. Mfano, madini ya kinywe (graphite), jasi (gypsum), chokaa (limestone), kaolini (kaolin) yanahitajika kwa wingi katika kuchochea uzalishaji wa bidhaa za viwandani.



Edit with WPS Office

Aidha, mafuta na gesi asilia, makaa ya mawe, maji, joto ardhi na urani ni rasilimiali zilizo katika miamba na zinahitajika sana katika kuzalisha nishati ambayo matumizi yake makubwa ni uzalishaji katika viwanda. Wajiolojia mnalo jukumu la kutuonyesha ni wapi maliasili hizi zinapatikana na kwa kiwango gani ili wazalishaji wa bidhaa za viwandani waweze kupata malighafi hizi kwa urahisi ili kuongeza tija katika viwanda vyetu hapa nchini.

**Ndugu Wajiolojia na wageni waalikwa,**
Katika Sekta ya Madini, nchi yetu imebarikiwa sana kuwa na madini mbalimbali, na mengi, mfano ni madini ya dhahabu ambayo yanachimbwa maeneo mbalimbali. Bado kuna viashiria vingi vinavyoonyesha dhahabu inapatikana maeneo mengine mengi hapa nchini. Mbali na dhahabu, tuna shaba, nikeli, kinywe (graphite) na madini mengine mengi ambayo siwezi kumaliza kuyataja hapa.

Vile vile, tuna madini ya vito ya aina mbalimbali, mfano mzuri ni Tanzanite inayopatikana Tanzania pekee, rubi na almasi ambayo yanachimbwa kwa wingi nchini. Madini yote haya yanaonyesha dhahiri kuwa nchi yetu imebarikiwa kuwa na rasilimali madini kwa kiasi kikubwa. Sisi ni moja ya nchi chache diniani tuliobarikiwa kuwa na rasilimali hizi kwa wingi. Hivyo, haishangazi katika kila mijadala ya maliasili duniani ikiwemo madini, Tanzania haiachi kutajwa.

Sisi kama nchi tumejidhatiti kuhakikisha maliasili hizi zinalinufaisha taifa kupitia usimamizi madhubuti. Kama mnavyofahamu, Serikali ilifanya mabadiliko makubwa katika Sheria ya Madini na kuanzisha Tume ya Madini (Mining Commission), kuboresha utendaji wa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (Geolocical Survey of Tanzania, GST) na kuliimarisha Shirika letu la Madini Tanzania (State Mining



Edit with WPS Office

Corporation, STAMICO).

Taasisi zote hizi kwa ujumla wake zimewezesha mchango wa sekta ya madini kuongezeka na kufikia asilimia 7.3 mwaka 2021 kutoka asilimia 3.8 mwaka 2014. Aidha, ushiriki wa Taifa letu kwenye shughuli za uchimbaji na mnyororo mzima kwenye sekta ya madini kupitia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) linazidi kuimarika na sote ni mashahidi juu ya mafanikio makubwa yaliyoadhimishwa wakati wa kumbukizi ya miaka hamsini (50) ya STAMICO mwaka huu, ambayo nilibahatika pia kuwa mgeni rasmi.

**Ndugu Wajiolojia,**
Vivyo hivyo, katika sekta ya nishati juhudi ni kubwa. Mbali na miradi mikubwa ya kufua umeme ukiwemo mradi wa Mwl. Nyerere *Hydropower Project* ambao nimejulishwa kuwa mlipata bahati ya ku-utembelea mwaka jana na kuona maendeleo yake, serikali imejenga na inaendelea kujenga vituo vikubwa vya kufua umeme kwa kutumia gesi asilia pamoja na ule wa maji Rusumo.

Joto ardhi pia ni kipaumbele kwa serikali ili sekta hii nayo ianze kuchangia katika nishati katika miaka ya hivi karibuni. Kampuni yetu ya Maendeleo ya Joto ardhi, ***Tanzania Geothermal Development Company (TGDC)*** kwa sasa imefikia hatua nzuri katika kufanya uhakiki wa kiwango cha joto ardhi (Resource confirmation) katika miradi mitano ya Ngozi, Kyejo Mbaka, Songwe, Luhoi na Natron. Na inatarajiwa kufikia mwaka 2025 miradi hii iweze kuchangia walau Megawati 200.

**Ndugu Wajiolojia,**
Mbali na joto ardhi, tumebarikiwa kuwa na mabonde yenye kuashiria kuwa vyanzo vya upatikanaji wa mafuta na gesi asilia. Tayari tumegundua kiasi kikubwa cha gesi katika mabonde



Edit with WPS Office

mbalimbali nchini ikiwemo sehemu ya bahari yetu ya kina kirefu, utafiti unaendelea kwenye mabonde mablimbali ikiwemo Bonde la Eyasi-Wembere na pia tumeanza kutumia gesi asilia katika viwanda vyetu nchini. Kwa sasa Gesi asilia inachangia uzalishaji wa umeme, takribani asilimia 70 ya umeme wote nchini.

Aidha, Serikali imekwishafanya mazungumzo na kusaini mkataba wa awali, ***Host Governemnt Agreement*** na makampuni makubwa ya uchimbaji wa gesi asilia juu ya uendelezaji wa gesi asilia (Liquefied Natural Gas, LNG) katika Mkoa wa Lindi. Uzalishaji huu utapoanza, nchi itapunguza utegemezi katika gesi asilia kwa ajili ya uzalishaji umeme na matumizi ya viwanda na majumbani na kuuza ziada nje ya nchi.

Pamoja na maendeleo yote haya, tafiti bado zinahitajika ili uvumbuzi huu uendelee na tupate gesi asilia nyingi zaidi pamoja na mafuta. Hili ni jukumu lenu wanajiolojia katika kuhakikisha tunafikia malengo haya.

Natambua pia tunayo madini mengi ya urani (uranium) sehemu kadhaa nchini, haya pia hutumika kuzalisha umeme. Huku tukijua tunatakiwa tufikie kuzalisha umeme mwingi na wa kiwango cha uhakika, hatuna budi kufikiria kufua umeme kwa kutumia rasilimali madini haya pindi tutakapopata uwezo unaotakiwa.

**Ndugu Wajiolojia,**
Pamoja na maji kutumika katika uzalishaji wa nishati, sote tunafahamu kuwa maji ni muhimu kwa matumizi ya majumbani na kwa matumizi mengine katika viwanda yasiyo ya uzalishaji nishati. Huwezi kuwa na viwanda vinavyozalisha kwa wingi na kwa tija bila kuwa na maji ya kutosha, na hakuna kiwanda kisichotumia maji. Kwa bahati nzuri maji ya miamba ni mengi sana na yanapatikana kila mahali hapa nchini kwetu. Utafiti wa



Edit with WPS Office

maji chini ya ardhi unahitajika sana wakati huu dunia inapokabiriwa na mabadiliko ya tabia nchi na hivyo maeneo mengi kukumbwa na ukame.

Vyanzo vya maji juu ya ardhi vimeharibiwa na vingine kukauka na maji chini ya ardhi yanatakiwa kuvunwa ili kutoa huduma kwa wananchi na viwanda. Hivyo basi, kiwanda kinaweza kuanzishwa mahali popote hapa nchini na kikapata maji ya kutosha kwa sababu maji yapo ardhini kila mahali. Nyie Wajiolojia ndio wa kutuonyesha wapi maji haya yanapatikana, na ikiwezekana tuwe na takwimu nzuri yenye kuonyesha kiwango cha maji, mahali yalipo na kwa ujazo gani. Takwimu hizi zikiwepo kwa nchi nzima tutakuwa tumerahisisha na kuvutia uwekezaji wa viwanda kote nchini. Muwekezaji wa kiwanda atakuwa na uhuru wa kuanzisha kiwanda sehemu yoyote ambayo kuna malighafi anayohitaji na hapo hapo ana uhakika wa kupata maji.

**Ndugu Wajiolojia,**
Kama mnavyofahamu, uwekezaji mkubwa katika uchumi wowote duniani unahusisha ushirikiano mzuri baina ya Serikali na Sekta Binafsi. Serikali ya awamu ya sita chini ya **Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, imeweka kipaumbele katika kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini mwetu ili kuvuta mitaji mikubwa kutoka ndani na nje ya nchi. Ni mategemeo yangu, wanufaika wakubwa wa sera hii ya kufungua milango zaidi kwa uwekezaji watakuwa ni wajiolojia na hivyo sishangai kuona Warsha yenu ya mwaka huu inaongozwa na kauli mbiu isemayo **“Mikakati ya kutenengeneza mazingira wezeshi ya uwekezaji katika sekta ya uziduaji” (Strategies in Creating Conducive Investment Environment in Extractive Industry).**

Kauli mbiu hii inakwenda sambamba na mwelekeo wa Sera na Utendaji wa Serikali ya Awamu ya Sita katika kuondoa vikwazo vya uwekezaji na hivyo kurahisisha mazingira ya kuanzisha



Edit with WPS Office

biashara ikiwemo biashara ya utafiti na uchimbaji wa rasilimali madini, mafuta na gesi asilia pamoja na maliasili zingine. Aidha, kauli mbiu hii inalenga kuwaleta wajiolojia pamoja ili kujadili namna bora zaidi ya kuwezesha uwekezaji katika sekta mnazohusiana nazo. Naomba kusisitiza kila mmoja kushiriki kikamilifu ili maazimio mtakayoyafikia muweze kuyawasilisha Serikalini na sisi tupo tayari kuyapokea na kuyafanyia kazi ili kuinua sekta ya uziduaji.

**Ndugu Wajiolojia,**
Pamoja na mijadala mtakayofanya inayolenga kauli mbiu yenu, pia mnayo nafasi ya kujiuliza swali muhimu kama Wajiolojia. Swali hili ni nyie Wajiolojia katika kuunga juhudi za maendeleo ya nchi yenu, jukumu lenu ni lipi?
Mnapaswa kuongeza juhudi katika utafutaji wa madini, joto ardhi, maji na mafuta na gesi asilia hapa nchini, tunataka migodi mingine mikubwa ifunguliwe sababu mbali na kuiongezea nchi kipato kutokana na mapato ya kodi na gawio, migodi hii itazalisha ajira. Utaalamu wenu unategemewa, na serikali inatambua umuhimu wenu. Sasa kwa uzalendo mlionao na utaalamu wenu, ebu ongezeni juhudi ili tuone idadi ya migodi midogo kwa mikubwa inaongezeka, ugunduzi zaidi wa mafuta na gesi asilia ukifanyika, maji ya ardhini yanagunduliwa na kuvunwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali, na joto ardhi linavunwa na kutumika kuzalisha umeme.

Serikali kwa kutambua umuhimu wa utaalamu wa kijiolojia nchini, bado inahakikisha vijana wakitanzania wanasomeshwa ili wapate utaalamu huu. Nchi yetu hii iliyojaliwa rasilimali madini, mafuta, gesi asilia, joto ardhi na maji ya ardhini, ni kubwa na kwa kiasi kikubwa bado nyie kama wajiolojia hamjatafiti sehemu kubwa ya nchi na hivyo bado migodi mingi haijagunduliwa.



Edit with WPS Office

Tutaendelea kufanya juhudi za kuwatengenezea mazingira mazuri ya kazi na kwa taasisi zetu tutaziwezesha kwa vitendea kazi vinavyohitajika ili haya yote tunayoyataka kutoka kwenu muweze kuyafanya kwa ufasaha.

**Ndugu Wajiolojia,**

**Uanzishwaji wa Bodi ya Usajili wa Wanajiosayansi**

Nimesikia changamoto mlizonazo, la msingi nililoliona na ambalo ni muhimu hasa katika kipindi hiki serikali yetu pamoja na serikali zote duniani, zinapopambana katika kuhakikisha zinatumia rasilimali zilizopo katika kuharakisha maendeleo kwa nchi na watu wake. Matumizi ya rasilimali ili yawe na tija sharti yasimamiwe kwa uadilifu mkubwa na hasa ikizingatiwa kuwa rasilimali mnazozihusiana nazo ni za thamani kubwa na hivyo kuvutia udanganyifu mwingi. Hivyo, ni muhimu kama wajiolojia na wanajiosayansi wote kwa ujumla kuwa na chombo kitakachosimamia taaluma hii muhimu.

Aidha, mchakato wa kutengeneza chombo hiki kitakachojulikana kama **Bodi ya Usajili wa Wanajiosayansi (The Geoscientists Registration Board, GRB)** umeanza na unaendelea katika Mamlaka mbalimbali za Serikali ili kuondoa tatizo la Sekta ya Uziduaji mikononi mwa wanataaluma wasiosimamiwa kama zilivyo taaluma kama za uhandisi, upimaji, uthaminishaji na taaluma zingine ambazo tayari wanazo bodi zao.

Hivyo, Wizara ya Madini inafuatilia taratibu za ukamilishaji wa mchakato wa kuundwa kwa Bodi hii ili Sekta za Nishati, Madini, Maji na zingine mnazohusiana nazo ziweze kusimamiwa kwa weledi kwa manufaa ya nchi.

Natambua bodi hii inayo umuhimu mkubwa hasa katika kusimamia maendeleo yenu kitaalamu na kiutendaji ili wakati



Edit with WPS Office

mnatimiza majukumu yenu muwe mnazingatia maadili na misingi ya utaalamu huu adhimu. Lakini pia bodi hii itakuwa chombo kitachosimamia vyema maslahi mapana ya utaalamu wenu hapa nchini, mfano, bodi iweze kulinda ajira za watanzania huku ikisaidia kusimamia sheria zetu katika Sekta zote mnazohusiana nazo kwa wawekezaji wa watendaji.

**Ndugu Wajiolojia,**
Katika utendaji wenu wa kazi, nyie ndio mtakuwa watanzania wa kwanza kujua kinachoendelea katika Sekta zote mnazohusiana nazo, yaani madini, maji na mafuta.

Haijalishi unafanya kazi Serikalini au Shirika binafsi, wewe ukiwa kama mtanzania una jukumu la kulinda rasilimali za nchi. Usijihusishe na usishiriki katika kulihujumu Taifa, kwani wewe utakuwa msaliti wetu namba moja. Ikiwezekana wewe ndio uwe balozi wa Serikali katika mashirika haya kwa kutoa elimu juu ya Sheria zinazosimamia Sekta hizi huku ukitoa msisitizo wa mashirika haya kufuata sheria hii.

Endapo kila mmoja wetu atafanya hivyo tutakuwa tumetoa mchango wetu katika taifa, hivyo maendeleo yanayotarajiwa kutokana na Sekta za Rasilimali Madini, Joto Ardhi, Mafuta na Gesi asilia yataonekana. Na nisisitize kwamba, **Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** haitakuwa na uvumilivu kwa yeyote atakayeshiriki kulihujumu taifa, ikigundulika kuna mwenzetu sio muaminifu basi huyo ndie atakayekuwa wa kwanza kufikishwa katika vyombo vya Sheria.

**Ndugu Wajiolojia**, **ndugu wageni waalikwa**,
Kwa kumalizia, naomba nisistize umuhimu wa kutathmini mchango wenu katika maendeleo ya nchi hii, hususani katika maendeleo ya sera katika Sekta ya Uziduaji.



Edit with WPS Office

Ni matumaini yangu na ni matumaini ya watanzania wote, kwamba mkitoka katika warsha hii kila mmoja wenu atakuwa ameijua nafasi yake katika maendeleo ya nchi.

Hivyo basi, nimalize kwa kuwatakia majadiliano mema na uelewa mpana wa taaluma na utaalamu wenu, huku nikiwa na matumaini mtaleta mabadiliko katika sekta hizi mnazohusiana nazo, pamoja na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Mwisho sasa kwa niaba ya Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania naomba NITAMKE RASMI KUWA MKUTANO MKUU WA MWAKA 2022 WA WAJIOLOJIA TANZANIA, **UMEFUNGULIWA RASMI**,

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA



Edit with WPS Office